



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI MASASI

**TANGAZO LA ZABUNI YA UPANGISHAJI JENGO LA MEF**  
**ZABUNI NA.LGA/135/2023/2024/MTC/NC/07**

Tarehe: 10.10.2023

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Halmashauri ya Mji Masasi inakusudia kutafuta mpangaji katika jengo la MEF.
2. Halmashauri ya Mji Masasi sasa inakaribisha Kampuni, Taasisi, Kikundi au watu binafsi wenye uwezo wa kuomba zabuni ya kupangisha jengo la MEF.
3. Mwombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo;
  - i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea mwenye kitambulisho cha Taifa.
  - ii. Mwombaji atataja aina ya biashara atakayoifanya na kodi ya pango anayokusudia kulipa kwa mwezi.
  - iii. Mwombaji aambatishe nyaraka za leseni hai ya biashara inayoendana na aina ya biashara/huduma anayokusudia kuitoa yaani leseni ya biashara, Namba ya utambulisho wa mlipa kodi n.k
  - iv. Kampuni/kikundi/Taasisi ziambatishe hati ya nguvu ya kisheria (power of Attorney)
  - v. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo,  
Mkurugenzi,  
Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 447,  
**Masasi.**

- vi. Maombi yafungwe vizuri kwa bahasha yenye rakili kisha yawasilishwe kwa mkono katika chumba Na.6, Ofisi ya Katibu wa Bodi ya zabuni, Halmashauri ya Mji Masasi, kabla ya tarehe 30.10.2023 saa 4.00 Asubuhi.
- vii. Waombaji wanaruhusiwa kufika katika ofisi ya Halmashauri ya Mji Masasi kwa ajili ya kukagua jengo linalokusudiwa kupangishwa katika siku na masaa ya kazi kuanzia saa 1.30 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri (Jumatatu-ijumaa)
- viii. Maombi yatakayochelewa,yatakayowasilishwa kwa njia ya posta/ barua pepe hayatapokelewa na hayatashughulukiwa.



Reuben S. Jichabu.  
Mkurugenzi wa Mji,  
**Masasi.**

